**TAARIFA FUPI YA WILAYA YA KARAGWE KWA MHESHIMIWA CHARLES TIZEBA (MB), WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA KATIKA ZIARA YAKE WILAYANI KARAGWE**

**TAREHE 16.02.2018**

**1. ULINZI NA USALAMA:**

Mheshimiwa Waziri,

Hali ya Ulinzi na Usalama kwa ujumla ni shwari, mipaka yetu na nchi jirani ni salama. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na raia linaendelea kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu kadiri yanavyotokea. Wilaya inajipanga kuanza zoezi la uandikishaji vitambulisho vya Taifa maandalizi yote yamekamilika tumepokea vifaa kutoka NIDA

Wilaya ya Karagwe inaundwa na tarafa za Bugene, Nyaishozi, Nyabiyonza, Kituntu na Nyakakika zenye jumla ya kata 23 na vijiji 77 vyenye jumla ya wakazi 332,020. Kaya zilizopo ni 72,830 na Kaya zinazoshiriki kilimo ni 61,351 ambazo ni 84.5%. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 108,000.

**2. HALI YA UTUMISHI IDARA YA KILIMO**

Idadi ya watumishi wa idara ya kilimo, Umwagiliaji na Ushirika waliopo makao makuu, kwenye kata na vijiji ni 60**.** Wiki hii tumepokea wataalam wawili wa kilimo toka Serikalini ambao wote wana elimu ya ngazi ya diploma.

Mgawanyo wa watumishi kwa taaluma zao.

| S/N | WATUMISHI KWA KADA ZAO | WALIOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| 1 | Mkuu wa idara ya kilimo | 0 | 1 |
| 2 | Watumishi wa kada ya ushirika | 2 | 4 |
| 3 | Watumishi wa kada ya kilimo mazao (Agriculture General) | 45 | 41 |
| 4 | Watumishi wa kada ya kilimo ugani (Agriculture Education & Extension) | 6 | 0 |
| 5 | Watumishi wa kada ya Uhandisi kilimo (Agro –engineers) | 4 | 2 |
| 6 | Watumishi wenye kada ya Matumizi bora ya Ardhi (udongo) | 1 | 2 |
| 7 | Watumishi wenye kada za Lishe | 1 | 1 |
| 8 | Watumishi wenye kada ya Mboga mboga na matunda | 1 | 2 |
| | | 60 | 53 |

Kwa agizo la Waziri mkuu la kubaki na wataalam watatu ofisini na wengine kupangiwa kwenye kata na Vijiji agizo hilo limezingatiwa na tayari maafisa ugani 7 waliokuwa makao makuu wamehamishiwa kwenye vituo vipya ili wakasimamie wakulima kwa karibu na kuleta ufanisi.

## 4. HALI YA CHAKULA WILAYANI

Katika wilaya ya Karagwe, kwa kipindi hiki cha mwezi Februari 2018, ambapo mazao mengi yameanza kuvunwa,hali ya chakula ni nzuri,maana chakula kipo cha kutosha na chakula cha ziada kinauzwa katika wilaya na mikoa ya jirani,na bei za vyakula mbalimbali vijijini na sokoni ziko chini kama zinavyoonekana kwenye jedwali lililoambatanishwa hapo chini.Pia jedwali la kiasi kilichozalishwa na kiasi cha chakula kinachohitajika limeambatanishwa.

### *4.1 BEI YA MAZAO MBALIMBALI SOKONI:*

| S/N | AINA YA CHAKULA | KIPIMO | BEI YA CHINI (Tshs) | BEI YA JUU (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ndizi | Mkungu | 3,000 | 15,000 |
| 2. | Mahindi | Debe | 6,000 | 10,000 |
| 3. | Mchele | Kg | 2,000 | 2,500 |
| 4. | Ngano | Kg | 1,400 | 1,500 |
| 5. | Ulezi | Kg | 2,500 | 3,000 |
| 6. | Mhogo mbichi | Kg | 1,000 | 1,500 |
| 7. | Viazi mviringo | Debe | 3,000 | 5,000 |
| 8. | Maharage | Kg | 1,000 | 1,500 |
| 9. | Viazi vitamu | Kg | 500 | 1000 |
| 10 | Viazi vikuu | Kg | 500 | 1000 |
| 11 | Nyanya | Kg | 700 | 1,000 |
| 12 | Mchicha | Fungu | 250 | 500 |
| 13 | Nanasi | Kila | 500 | 1000 |
| 14 | Karanga | Kilo | 1000 | 1500 |

### 4.2 Hali ya upatikanaji wa chakula; februari 2018

| Idadi ya watu | Mahitaji ya chakula (T) | Upatikanaji (T) | Ziada (T) | Upungufu (T) |
|---|---|---|---|---|
| 332,020 | 78,000 | 348,948 | 270,948 | Hakuna |
| | | | | |

## 5. UPATIKANAJI WA PEMBEJEO ZA KILIMO NA ZANA

### 5.1 MBOLEA

Kwa mujibu wa waraka wa Wizara ya Kilimo uliotolewa hivi karibuni kwa mwaka 2017/18 Serikali imebadili mfumo wa utoaji ruzuku ya pembejeo za kilimo tofauti na utaratibu wa vocha ilivyozoeleka. Kwa sasa mfumo unaotumika ni Serikali kufidia moja

kwa moja bei ya mbolea; hivyo wauzaji wa mbolea wanauza bidhaa hii kwa bei elekezi ambayo hutolewa kila mwezi na kwa Karagwe bei elekezi ya mbolea ya kupandia (DAP) kwa mwezi February ni Tshs.57,771/= kwa mfuko wa kilo 50 tofauti na bei ya soko ya Tshs.68,000/= punguzo la 18% na mbolea ya kukuzia (UREA) itauzwa kwa bei ya Tshs.45,317/= kwa mfuko wa kilo 50 tofauti na bei ya soko ya Tshs.54,667/= punguzo la 20%. Hii yote inatokana na umbali wa barabara toka Dar es Salaam ambazo ni kilomita 1,640
Imetolewa na *Tanzania Fertilizer Regulatory Authority.*

Kwa Wilaya yetu ya Karagwe mawakala wanaojihusisha na ununuzi na uuzaji wa pembejeo wameshindwa kunufaika na mfumo huu wa (Bulk) na hii imesababishwa na ukosefu wa mitaji na matumizi madogo ya mbolea.

**Jedwali; UTEKELEZAJI HADI SASA**

| **Mbolea ya Kupandia** | | **Mbolea ya kukuzia** | | **Mbegu bora za Mahindi** | | **Mpunga (Kg)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.DAP (T) | 9.5 | UREA (T) | 7.4 | Chotara (T) | 1.6 | |
| 2.Jumla ya Mbolea nyingine za viwandani za kupandia (T) | 2.1 | Jumla ya Mbolea nyingine za viwandani za kukuzia (T) | 0.8 | OPV (T) | 13.4 | |
| 3. Mbolea za asili (**SAMADI**) (T) | 63.7 | | | | | |

## 5.2 MBEGU

Hali ya upatikanaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali ya nafaka kama mahindi, maharagwe, karanga nk imekuwa tete kwa muda mrefu sasa hali inayowafanya wakulima kuendelea kupanda mbegu zenye uzao hafifu na hivyo kusababisha uzalishaji duni kwa wakulima wetu. Maduka ya pembejeo yaliyopo yanazo mbegu kidogo ambazo hazitoshelezi mahitaji ya wakulima. Hata hivyo mbegu zinazoletwa zinakuwa na bei kubwa ambapo wakulima wengi wanashindwa kumudu.

Bei za mbegu za mazao ni kama ifuatavyo;-

- Mbegu za mahindi (hybrids) ziliuzwa kati ya Tshs.10,500/= hadi 12,000/= kwa mfuko wa kilo 2
- Mbegu za mahindi (msingi) ziliuzwa kati ya Tshs.6,000/= hadi 8,000/= kwa mfuko wa kilo 2
- Mbegu za maharage (Hybrids) mf. Lyamungo 90 zinauzwa kwa Tshs 3,000/= hadi 4,500/= kwa kilo

- Mbegu za kahawa (miche) iliuzwa kwa bei ya kati ya Tshs.300/=kwa mche hadi Tshs.500/=kwa mche. Isipokuwa kwa miche yote iliyozalishwa kwenye vitalu vinavyomilikiwa na taasisi ya Utafiti wa kahawa TACRI miche 13,000 iligawiwa bure kwa wakulima.
- Mbegu za mihogo ziliuzwa kwa bei kati ya Tshs.20-30 kwa pingili na zinapatikana kwa wakulima wazalishaji
- Mbegu za viazi lishe zinapatikana kwa wakulima wa Vijiji vya Kishoju, Chabuhora na Bujuruga na ziliuzwa kwa bei ya Tshs.16 kwa pingili.

## 6. TAARIFA YA ZAO LA KAHAWA

Idara imeendelea kusimamia ukusanyaji wa takwimu za ununuzi wa kahawa kutoka kwenye makampuni yanayonunua kahawa kwa msimu wa 2017/2018 ambapo hadi kufikia mwezi Disemba, 2017 jumla ya Kg. 3,051,483 sawa na Tani 3,051.5 za kahawa ya maganda zimekusanywa na kampuni saba zilizojitokeza kununua kahawa wilayani Karagwe kwa msimu wa 2017/18 kama mchanganuo unavyojionyesha hapa chini;-

**Jedwali; Taarifa ya ununuzi wa Kahawa msimu 2017/2018 hadi kufikia mwezi Disemba, 2017.**

| S/N | JINA LA KAMPUNI | KIASI NUNULIWA (KILO) | | JUMLA YA KILO | BEI YA KUNUNULIA (T.shs) | KIASI KOBOLEWA (KILO) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ARABICA | ROBUSTA | | | |
| 1 | KARAGWE ESTATE Co. LTD | | 1,382,244 | 1,382,244 | 1550-1800/= | 1,382,244 |
| 2 | EXPORT TRADING Co.LTD | | 265,659 | 265,659 | 1600-1800/= | 265,659 |
| 3 | OLAM (T) LTD | | 808,598 | 808,598 | 1550-1800/= | 808,598 |
| 4 | KDCU LTD | 47,020 | 175,239 | 222,259 | 1400-1600/= | 222,259 |
| 5 | AMRI AMIR ALHABSY CO.LTD | | 240,119 | 240,119 | 1650-1800 /= | 240,119 |
| 6 | KADERES PLC | | 78,604 | 78,604 | 1700-1800/= | 78,604 |
| 7 | LION WATTLE(T) LTD | | 54,000 | 54,000 | 1600/= | 54,000 |
| **TOTAL** | | **47,020** | **3,004,463** | **3,051,483** | | **3,051,483** |

NB; Uzalishaji wa kahawa umeshuka kutoka kilo 9,819,000 sawa na tani (9,819) za msimu uliopita wa 2016/2017 hadi kilo 3,051,483 za msimu huu wa 2017/18 sawa na upungufu wa 70% kutokana na athari za ukame ulioikumba Wilaya ya Karagwe na kusababisha mikahawa mingi kunyauka na mingine kukauka, na hivyo kuathiri mapato ya ndani. Pia mapato yameathiriwa na kushuka kwa ushuru (coffee cess) kutoka 5% hadi 3%.

Hata hivyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya wilaya imepanga Tshs.100,000,000/= kwenye bajeti ya mapato ya ndani kwa ajili ya kununulia miche ya kahawa na kuigawa kwa wakulima bure

## 7. UTEKELEZAJI WA MALENGO YA KILIMO KWA MWAKA WA 2017/2018

| | **ENEO LIMWA (Ha)** | **JUMLA YA MAVUNO TARAJIWA KWA ENEO (TANI)/Ha** |
|---|---|---|
| Ndizi mbichi | 51,717.5 | 1,022,015 |
| Mazao ya Nafaka | 77,888.9 | 133,817.04 |
| Mazao ya mizizi | 20,763.1 | 174,545.7 |
| Mazao ya biashara | 21,401.5 | 43,168.1 |
| Matunda na mbogamboga | 2432.6 | 22,245.9 |
| **Jumla** | **174,203.6** | **1,395,791.74** |

## 8. TAARIFA YA KITENGO CHA USHIRIKA

Kitengo cha Ushirika kina watumishi wawili (2) tu .Wilaya ya Karagwe inavyo vyama vya Ushirika aina nne 1. Chama Kikuu cha Ushirika –KDCU LTD kimoja 2. Agricultural Marketing Cooperative Society (AMCOS) 37, 3. Savings and Credit Cooperative Societies (SACCOS) 33 na 4. Vyama vingine 5 (Wafugaji, Wazalishaji na wanunuzi wa kahawa)

Wilaya kwa muda mrefu imekuwa ikikabiliwa na tatizo sugu la uuzaji wa kahawa ikiwa bado iko shambani maarufu kama BUTURA na kuharibu ubora wa kahawa.
Baada ya Mh. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuagiza kahawa yote inunuliwe sokoni na kuzuia wafanya biashara binafsi wasinunue kahawa kwa wakulima, Mh.Waziri wa Kilimo nakuhakikishia wakulima wamepata faraja sana kwa wazo hili la Serikali na mimi kama Mkuu wa Wilaya nalisimamia vizuri bila kutetereka.

Tumefanya mikutano ya hadhara kwenye maeneo ya Nyabiyonza, Kituntu, Nyaishozi, Nyakabanga, Rugu na Kiruruma. Pia elimu zaidi inatolewa kupitia Radio zetu za Karagwe FM na FADECO Radio. Kwa sasa Wataalam wa idara ya kilimo kwa kushirikiana na chama kikuu cha Ushirika KDCU LTD wanaendelea kukusanya takwimu muhimu zinazohusu wakulima wa zao la kahawa ili kuwa na kanzi data(data base) itakayosaidia uratibu na huduma bora kwa wakulima wa zao hili.

## 9. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UGANI

Ili wakulima wapate ushauri wa kitaalam kwa urahisi na kusambaza teknolojia mbalimbali kwa urahisi idara imeanzisha mashamba ya mfano na ya uzalishaji wa

mbegu kwenye maeneo mbalimbali ya wilaya. Pia kila afisa ugani amepewa daftari la bwana shamba ambalo linamsaidia kwa kazi zake za kila siku. Kila wiki wanatoa taarifa ya utekelezaji.

**VITENDEA KAZI**

| WATUMISHI | GARI | PIKIPIKI | MIKASI | MISUMEMO | EXTENSION KIT |
|---|---|---|---|---|---|
| 60 | 1 | 17 | 0 | 4 | 0 |

Wilaya ina upungufu vya vifaa kwa ajili ya kuwawezesha wataalam; pikipiki 43, mikasi 58 misumeno 54 na extension kit 58.

**CHANGAMOTO ZINAZOKABILI IDARA YA KILIMO**

- Mabadiliko ya tabia nchi yanasababisha hali ya ukame kwa baadhi ya maeneo
- Magonjwa ya mimea kama vile ugonjwa wa Unyanjano, Ugonjwa wa batobato kali
- Upungufu wa watumishi wa kada za chini umesababishia idara kushindwa kuwafikia wakulima wengi na kuwapa huduma za kitaalam
- Ukosefu wa mafunzo rejea, ukosefu wa vitendea kazi na uwezeshwaji wa vifaa muhimu kama mikasi, misumeno, n.k

**UTATUZI WA CHANGAMOTO**

- Kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa idara imehimiza wakulima kulima mazao ya kinga ya njaa kama viazi na mihogo, kupitia wagani na Radio zilizopo Wilayani
- Idara inaendelea kutoa mafunzo rejea kwa wataalam wa ugani ili waendane na wakati

Naomba kuwasilisha

**MAKUNENGE MANYANGELE**
**KAIMU; KATIBU TAWALA (W)**
**<u>KARAGWE</u>**